

**Dondoo za mkutano wa Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam
24 January 2009**

Waliohudhuria

Ally Saidi Mwishehe
Bashiri Rashidi
Beda John Mkusu
Elaine Baker
Filbert Mbecha
Hamadi Hatibu Bwaja
Juma Ali Salehe Jongo
Juma Hassan Chibaya
Kassim Bakari
Kibwana Mohammad Msiga
Mussa Alex
Paulo Atibu Hatibu
Rashidi Saidi Karanji
Selion Elieskia
Shamte J Kigoma
Shukuru Hassan
Sosthenes C Amlima
Sudi Saidi Ramadhan

Sherehe ya walemavu

Juma Jongo, Juma Chibaya, Maximilian na Kibwana walihudhuria sherehe ya walemavu jumapili na walisambaza vipeperushi kuhusu UWABA kwa wapanda baisikeli walemavu.

Ushirika wa kibarua wa baisikeli

Idrisi hajaja mikutano kutuambia kama amekutana na ofisa ya ushirika. Shukuru alisema ataenda kutana na ofisa.

Mradi wa Wamba

Mwalimu Emmanuel wa Shule ya Kigamboni alipendekeza tufanye mafunzo mwezi wa pili kwa sababu bado wanafunzi wanaanza mwaka mpya. Una kutoka mfumo wa Wamba alisema atafuatalia sehemu ya pili ya fedha kwa UWABA wiki ijayo.

Video ya usalama wa baisikeli

Rafiki wa Elaine aliweza kutengeneza DVD kutoka film yetu. Hamadi na Sosthenes watakata taarifa kuhusu gharama za kupiga copy 30. Sosthenes alisema video ya msafara wa baisikeli 2007, ambayo tulifikiri imepotea na wafundi, imepatikana tena. Atajaribu kuipata.

Serikali ya jiji na kongamano

Ofisa wa jiji hajajibu SMS ya Elaine. Hajampigia simu kwa sababu atasafiri wiki hii na atapenda kuhudhuria mkutano.

Ruzuku ya Foundation for Civil Society

Elaine aliandaa barua kwa Bwana Wemba wa NIT, Bwana Gaja wa kampuni ya guta na Bwana Lupilya diwana kuwaomba wawe wadhamini huru wetu. Pia aliandaa barua kwa mtaa kuomba barua ya utambulisho. Wanachama walisahihisha barua na atatengeneza upya. Juma Chibaya atapeleka barua kwa Mtaa, Hamadi kwa Bwana Wemba na Paulo kwa Bwana Gaja na Bwana Lupilya.

Baiskeli kutoka UK

Elaine hajapata nafasi kutafuta taarifa zaidi kwenye intaneti – atafanya wiki hii.

Mambo ya hela na guta

Filbert alileta Tsh 7,000 hela ya guta. Juma alilipa Tsh 30,000 kwa kodi ya sanduka la posta. Tsh 5,200 ilitumika kufanya photocopy za vipeperushi na Tsh 3,200 kwa usafiri na chakula wa washiriki kwenye sherehe ya walemavu. Tsh 2,000 ilitoa kama advance kwa Elaine kuprint upya barua nne. Juma anabaki na Tsh 14,400 ya hela ya UWABA.

Mambo mengine

Elaine ataandaa kitambulisho cha Maximilian na ataleta kamera kuandaa vitambulisho vingine.